# TAMKO KUHUSU WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU

Azimio la Umoja wa Mataifa la mwaka 1998 kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu linafafanua Watetezi wa Haki za Binadamu kama "mtu au kikundi chochote ambacho, mtu binafsi au kwa taaluma yake, mtu mmoja mmoja, au akiwa na wengine, wanatenda kwa amani ili kulinda na kuendeleza haki za binadamu."

Sambamba na kulinda Haki za Binadamu, ni sera ya EACOP ya kuheshimu haki za uhuru wa kujieleza, uhuru wa kutangamana na uhuru wa kukusanyika kwa amani, pamoja na uhuru wa kupata taarifa katika ushirikiano wake na wadau walioguswa na shughuli za mradi.

EACOP inatambua uhalali na jukumu muhimu la Watetezi wa Haki za Binadamu (kama inavyoelezwa katika Azimio la Umoja wa Mataifa la mwaka 1998 kuhusu Watetezi wa Haki za Binadamu) katika kukuza na kulinda haki za binadamu, na zaidi ya hapo EACOP inatambua Ibara ya 38 na ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Uganda na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inayotoa haki kuhusu shughuli za kiraia. EACOP inatambua pia Nafasi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) iliyopitishwa mwaka 2018 kuhusu ulipizaji Kisasi dhidi ya Asasi ya Kiraia na Wadau wa Mradi.

**"Kulingana na viwango vya kimataifa vya Haki za Binadamu, EACOP haivumilii vitisho, unyanyasaji au uvunjaji wowote wa haki za binadamu dhidi ya wale wanaokuza kwa amani Haki za Binadamu zinazohusiana na shughuli zetu."**

EACOP inalenga kukuza mazungumzo na Watetezi wa Haki za Binadamu katika mfumo wa shughuli zake. EACOP inathamini ushirikiano na wadau wote kuhusiana na masuala yanayohusiana na Watetezi wa Haki za Binadamu na haki za kiraia. Inakaribisha maoni mahususi kutoka kwa wadau wanaotoa malalamiko au kutoa taarifa kuhusu matukio yanayohusiana na Watetezi wa Haki za Binadamu (na kutunza usiri wao). Kama sehemu ya ushirikiano wake undelevu kuhusu masuala haya, EACOP itaendelea kuweka mkazo mahususi kwa wanawake na makundi yaliyo katika mazingira magumu.

Pale Inapofaa, kama inavyopendekezwa na Kanuni Elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu kazi na Haki za Binadamu, EACOP inalenga kutumia uwezo wake kuwashawishi wengine kuheshimu kanuni hizi.

**Iwapo itaarifiwa uwapo wa madai ya vitisho, unyanyasaji au vurugu dhidi ya Watetezi wa Haki za Binadamu kutokana na shughuli zake, EACOP italazimika:**

- Kuchukua hatua za haraka ili kupata taarifa zaidi ili kuelewa aina ya hatari/madhara na kama yanahusiana na shughuli za EACOP.
- Kutunza usiri wa watu wanaohusika.
- Pale inapofaa, wasiliana na maafisa husika ambao wanaweza kuwa Mamlaka za polisi jamii, wilaya, kitaifa, Mamlaka ya Petroli ya Uganda (PAU) nchini Uganda na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) nchini Tanzania, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Uganda na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Tanzania, Tume ya Uganda ya Haki za Binadamu (UHRC) nchini Uganda, na Tume ya Tanzania ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG).
- Kusisitiza juu ya haja ya kuheshimu haki za binadamu za Watetezi wa Haki za Binadamu na hasa usalama, ulinzi, haki yao ya kusikilizwa katika mchakato wote wanapokabiliwa na mashitaka.
- Pale Inapofaa, kutoa taarifa kwa mashirika mengine ambayo yanaweza kujumuisha UHRC, CHRAGG, na Balozi husika, mashirika husika yasiyo ya kiserikali katika nchi zote mbili.
- Pale ambapo wafanyakazi au wakandarasi wa EACOP wanahusishwa na tuhuma hizo, hakikisha kwamba uchunguzi stahiki unafanyika kwa mujibu wa taratibu za EACOP, ikijumuisha kuchukua hatua za haraka na kuweka vikwazo stahiki.

**KUELEZA MADUKUDUKU AU MALAMIKO KAMA MTETEZI WA HAKI ZA BINADAMU**

***EACOP inahimiza matumizi ya Utaratibu wake wa Malalamiko na madukuduku ya aina zote yanayohusiana na shughuli zake ikiwa ni pamoja na Watetezi wa Haki za Binadamu.***

- EACOP ina Maafisa Uhusiano wa Jamii na maafisa uhusiano wasimamizi ambao mara kwa mara hutembelea maeneo yote ya shughuli zetu na kukutana na jamii, na wanaweza kuambiwa matatizo, kutoa mrejesho au malalamiko.
- Pia, EACOP ina namba ya kupiga bila malipo, ambayo ni (Uganda: 0800 113 205 na Tanzania: 0800 120 073) inayopatikana kila siku kuanzia saa 1 asubuhi hadi saa 4 usiku.
- Barua pepe

  Uganda: info.ug@eacop.com

  Tanzania: info.tz@eacop.com
- Mamlaka za ndani za kitamaduni/wilaya: malalamiko yanaweza pia kuibuliwa na viongozi wa kijamii kwa ajili ya kuyawasilisha EACOP.

EACOP inamhimiza Mtetezi yeyote wa Haki za Binadamu ambaye hatapendelea kuwasiliana na mradi moja kwa moja, kwa sababu za usiri au kutokujulikana, kuwasiliana na mtu mwingine ambaye atamchagua (k.m., Shirika Lisilo la Kiserikali, Ubalozi, n.k). Hawa watapeleka malalamiko yako kwa timu zetu kupitia utaratibu ulio hapo juu au kupitia barua pepe za EACOP zilizotajwa hapo juu.

**Guillaume DULOUT**
Mkurugenzi Msimamizi
Tarehe: May 2025